

[Namba: 4]

سُؤَالٌ وَجَوَابٌ

فِي

أَحْكَامِ الصِّيَامِ

SWALI NA JAWABU

KUHUSU

HUKUMU ZA SAUMU

Mtunzi:

Sheikh Muhammad Bin Swaleh Al-Uthaymin

Tarjama:

Abu Halima Arafat Bin Mahmoud

HUKUMU MBALIMBALI ZA MWENYE HEDHI NA NIFASI

Swali: Mwanamke mwenye hedhi au nifasi akitwahaarika katika mchana wa Ramadhani, je, ni wajibu wake kujizuia (katika masaa yaliyobaki)?

Jawabu: Si wajibu kwake kujizuia (katika masaa yaliyobaki), inajuzu kwake kula na kunywa, kwa sababu kujizuia kwake hakuna faida yoyote, kwa sababu ni wajibu wake kuilipa siku hiyo.

Swali: Ni ipi hukumu ya saumu/funga ya mwanamke mwenye hedhi ambaye ametwahaarika kabla ya kuchomoza alfajri, lakini amechelewa kuoga mpaka baada ya fajri?

Jawabu: Ikiwa mwanamke mwenye hedhi ametwahaarika kabla ya kuchomoza alfajri kwa dakika moja (muda mchache), lakini ameyakini kwamba ametwahaarika, ikiwa ni mwezi wa Ramadhani basi ni wajibu wake kufunga, na saumu/funga yake siku hiyo itakuwa ni sahihi, hata kama amechelewa kuoga mpaka baada ya kuchomoza alfajri, hapana vibaya.

Swali: Tangu nimewajibika kufunga Ramadhani ninafunga, lakini sijawahi kulipa masiku ambayo nimeacha kufunga kwa sababu ya mzunguko wangu wa mwezi (hedhi), na wala sijui (mpaka sasa) idadi ya siku ambazo nilifungua, tafadhali nielekeze nifanye nini hivi sasa?

Jawabu: Kwanza ni wajibu kwa mwanamke huyu atubu kwa Allaah na aombe msamaha kwa yale aliyoyafanya, na afuatilie siku ambazo ameacha kufunga kadri awezavyo kisha azilipe, na kufanya

hivi itakuwa jukumu lake limeondoka, na tunatumai kwamba Allaah atakubali toba yake (atamsamehe).

SAUMU/FUNGA YA MWANAMKE MWENYE MIMBA NA MWENYE KUNYONYESHA

Swali: Ni ipi hukumu ya mwanamke mwenye mimba au mwenye kunyonyesha, ambaye amekula mchana wa Ramadhani bila ya udhuru/sababu ya kisheria, hali ya kuwa ni mzima mwenye nguvu, na wala hapati madhara yoyote endapo atafunga?

Jawabu: Haifai kwa mwanamke mwenye mimba au kunyonyesha kula mchana wa Ramadhani isipokuwa kwa sababu za kisheria, na endapo atakula mchana (wa Ramadhani) kwa sababu za kisheria, itwajibika juu yake kulipa siku hiyo, kama alivyosema Allaah kuhusu mgonjwa: [Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi atimize hisabu katika siku nyingine]. Surat Al-Baqara/185. Nao pia hukumu yao ni sawa na mgonjwa.

SAUMU/FUNGA YA MTOTO MDOGO

Swali: Je, watoto walio chini ya miaka kumi na tano, wataamrisha kufunga kama wanavoamrisha kuswali?

Jawabu: Ndio, watoto ambao hawajifikia baleghe, wataamrisha kufunga ikiwa wataweza, kama Maswahaba wakivyofanya kwa watoto wao, lakini ikiwa (funga) ni ugumu kwao au inawadhuru, basi hawatalazimishwa kufanya hivyo.

NAMNA YA KULIPA SAUMU

Swali: Nini hukumu ya kuharakisha kulipa masiku ya Ramadhani?

Jawabu: Kuharakisha kulipa masiku ya Ramadhani ni bora zaidi kuliko kuchelewesha, kwa sababu mtu hajui nini kitamtokea, na kuharakisha kulipa deni la Ramadhani ni jambo zuri na kupupia katika kheri, wala haifai kwa mtu ambaye anawajibu wa kulipa siku za Ramadhani kuchelewesha mpaka kufikia Ramadhani nyingine bila ya sababu za kisheria.

Swali: Iwapo atachelewesha kulipa (funga ya) Ramadhani bila ya sababu za kisheria, kisha ikafika Ramadhani ya pili, je itamlazimu kutoa (fidia) pamoja na kulipa?

Jawabu: Kauli yenye nguvu ni kwamba, hakuna kinachomlazimu isipokuwa kulipa (siku alizoacha kufunga) tu, wala haimlazimu kutoa fidia, kwa kauli ya Allaah: [Na mwenye kuwa mgonjwa au safarini, basi atimize hisabu katika siku nyingine]. Surat Al-Baqara/185. Na ni haramu mtu kuchelewesha kulipa mpaka kuingia Ramadhani ya pili isipokuwa kwa sababu za kisheria.

Swali: Ni ipi hukumu ya mtu aliyekufa hali ya kuwa anawajibika kulipa siku alizoacha katika Ramadhani?

Jawabu: Iwapo mtu amekufa na hali ya kuwa anadaiwa siku za kufunga katika Ramadhani, basi walii wake (jamaa wa karibu) atafunga kwa niaba yake, kwa hadithi ya Aisha (Allaah amridhie), kwamba Mtume (Swala na Salamu zimshukie) amesema: [Mwenye kufa hali ya kuwa ana deni la saumu (ya wajibu), basi walii

wake atafunga kwa niaba yake]. Bukhari (1851) na Muslim (153 na 1147). Na kama hakufunga basi atoe fidia kwa kumlisha kila masikini mmoja kwa kuzingatia idadi ya masiku aliyoacha.

Tanbih: Saumu/funga ya wajibu ni kama vile: Ramadhani, Nadhiri, Kafara. Ikiwa mtu anadaiwa baadhi ya masiku katika mwezi wa Ramadhani, aliacha kufunga kwa sababu ya maradhi n.k, kisha baada ya kupona hakuwahi kulipa siku mpaka amefariki, basi jamaa zake wanahiyari baina ya kufunga kwa niaba yake au kulisha maskini. Kadhaalika mtu aliyeweka nadhiri au mwenye fungu ya kafara, jamaa zake watafunga au watalisha masikini.

Swala na Salamu zimshukie Mtume wetu, Jamaa zake na Maswahaba wote

Namuomba Allaah anitakabalie amali yangu hii na aiwafikishe

**Markaz Sheikhil Islaam Ibn Taymiyyah
19/sha'bani/1444H - 11/3/2023M
Pongwe Tanga.
Simu: 0715263253**